

Mbuzi, Mbwa na Ng'ombe

-  Fabian Wakholi
-  Marleen Visser, Ingrid Schechter
-  Brigid Simiyu
-  2
-  Kiswahili 



Mbuzi, Mbwa na Ng'ombe walikuwa marafiki wa karibu sana. Siku moja walisafiri kwa teksi.



Walipofika mwisho wa safari yao, dereva aliwaomba walipe nauli zao. Ng'ombe alilipa nauli yake.



Mbwa alilipa zaidi kidogo kwa sababu hakuwa na pesa taslimu.



Dereva alipokaribia kumpa Mbwa chenji yake,
Mbuzi alitoroka bila kulipa chochote.



Dereva alikasirika sana. Aliondoka bila kumrudishia Mbwa chenji yake.



Hiyo ndiyo sababu hadi leo Mbwa hukimbiza magari ili achungulie ndani kuona kama atampata dereva mwenye chenji yake.



Mbuzi hukimbia anaposikia mlio wa gari.
Anaogopa atakamatwa kwa kutolipa nauli.

Na Ng'ombe hababaiki gari likiwa linakuja.
Ng'ombe huvuka barabara bila wasiwasi kwa
sababu anajua alilipa nauli yake yote.



Global Storybooks

globalstorybooks.net

Mbuzi, Mbwa na Ng'ombe

✍ Fabian Wakholi

✉ Marleen Visser, Ingrid Schechter

☞ Brigid Simiyu

